**KAULI YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA ILIYOTOLEWA BUNGENI KUHUSU WATUMISHI WALIOONDOLEWA KWENYE MFUMO WA MALIPO YA MSHAHARA KWA KUKOSA SIFA YA CHETI CHA KUFAULU MTIHANI WA ELIMU YA KIDATO CHA NNE**

**Mheshimiwa Spika;**

Kufuatia kupitishwa na kuanza kutumika kwa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, Toleo la mwaka 1999 pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma (Public Service Act) Na.8 ya Mwaka 2002, Serikali iliweka sharti kwamba kiwango cha chini cha kuwezesha Mtumishi kuajiriwa katika Utumishi wa Umma ni kuwa na cheti cha kufaulu mtihani wa Kidato cha Nne.

**2.** Aidha kwa nyakati mbalimbali Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilitoa nyaraka kadhaa za kufafanua utekelezaji wa uamuzi huu kama ifuatavyo:-

**(a)** Nyaraka Mpya za Kada Mbalimbali za Maendeleo ya Utumishi wa Umma za Mwaka 2002 ambazo zilihuisha Utumishi wa Umma ili kuendana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma Toleo la Mwaka 1999 na Sheria ya Utumishi wa Umma (Public Service Act) Na.8 ya Mwaka 2002;

**(b)** Waraka wa Utumishi *(Establishment Circular)* Na. 1 wa mwaka 2004 kuhusu Utekelezaji wa Miundo ya Maendeleo ya Utumishi ya Mwaka 2002 ambao ulielekeza kwamba, Watumishi wa Umma ambao walikuwa katika ajira kabla ya tarehe 20 Mei, 2004, **hawatalazimika kujipatia sifa ya kuwa na cheti cha kufaulu mtihani wa kidato cha nne ili waendelee na ajira katika Utumishi wa Umma**;

**(c)** Barua ya Katibu Mkuu Utumishi yenye Kumb. Na. AC.45/260/01/86 ya tarehe 10 Aprili, 2006 ambayo pamoja na mambo mengine, ilibainisha kwamba ajira zote mpya hazina budi kufanyika kwa kuzingatia Miundo ya Maendeleo ya Utumishi iliyokuwa ikitumika wakati huo (**mwaka 2006)** ambayo moja ya vigezo vikuu ni **kuwa na cheti cha ufaulu wa mtihani wa kidato cha nne kama sifa ya msingi;**

**(d)** Barua ya Katibu Mkuu – TAMISEMI yenye Kumb. Na. CAB.58/337/01 ya tarehe 13 Julai, 2005 kuhusu Utekelezaji wa Ajira za Mkataba wa Miaka Mitatu Mitatu kwa Watendaji wa Vijiji na Mitaa. Barua hii iliwatambua **Watendaji wa Vijiji 3,940 waliokuwa na sifa na ambao hawakuwa na sifa** yaani wenye kiwango cha elimu ya msingi (Darasa la Saba) waliokuwa kwenye ajira ya mkataba kabla ya tarehe 20 Mei, 2004;

(e) Barua ya Katibu Mkuu Utumishi yenye Kumb. Na. CCB.271/431/01/P/13 ya tarehe 30 Juni, 2011, ambayo ilieleza kwamba baada ya Katibu Mkuu Kiongozi kupokea maombi kutoka kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokosa watumishi wenye sifa za miundo ikiwa ni pamoja na sifa ya kufaulu mtihani wa kidato cha nne, aliridhia ajira za Watumishi wa Kada mbalimbali wapatao Elfu Moja Mia Tatu Sabini **(1,370)** waajiriwe ili shughuli za Serikali zisiathirike katika Halmashauri husika.

(f) Barua ya Katibu Mkuu Utumishi yenye Kumb. Na. CFC.26/205/01 "G"/ 61 ya tarehe 10 Julai, 2017 kuhusu ufafanuzi wa Sharti/Sifa ya kuwa na cheti cha kufaulu mtihani wa kidato cha nne na cha sita katika ajira kwenye Utumishi wa Umma. Barua hii pamoja na mambo mengine ilisisitiza kwamba Watumishi wa Umma ambao walikuwa katika ajira kabla ya tarehe 20 Mei, 2004, **hawatalazimika kujipatia sifa ya kuwa na cheti cha kufaulu mtihani wa kidato cha nne ili waendelee na ajira katika Utumishi wa Umma** isipokuwa wale walioajiriwa baada ya tarehe 20 Mei, 2004 ambao Miundo yao ya Utumishi iliwataka kuwa na cheti cha kufaulu mtihani wa kidato cha nne na ambao hadi mwezi Julai, 2017 hawakuwa wamewasilisha vyeti vyao kuhakikiwa, **Mishahara yao isimamishwe kuanzia mwezi huo;**

**Mheshimiwa Spika;**

**3.** Kama mtakavyoona utekelezaji wa ajira katika Utumishi wa Umma tangu kuanza kutumika kwa miundo mipya umekuwa na tafsiri tofauti na ndiyo sababu barua nyingi za kutoa ufafanuzi zilitolewa kuanzia mwaka 2002 baada ya Serikali kubaini kwamba baadhi ya mamlaka za ajira zilikuwa zikiajiri watumishi wasiokuwa na sifa stahiki katika baadhi ya kada;

**Mheshimiwa Spika;**

**4.** Kufuatia hali hiyo, Serikali ilitoa maelekezo kupitia barua ya Katibu Mkuu Utumishi yenye Kumb.Na. CFC.26/205/01"Q"/61 ya tarehe 10 Julai, 2017 ikiwataka Waajiri kusimamisha mishahara ya watumishi waliaojiriwa baada ya tarehe 20 Mei, 2004 wakiwa hawana sifa ya kufaulu mtihani wa elimu ya kidato cha nne hadi watakapowasilisha vyeti husika. Katika zoezi hili, jumla ya Watumishi **7,382 (Watendaji wa Vijiji - 3,817, Watendaji wa Mitaa - 51, Watendaji wa Kata - 253, Madereva wa Magari - 330, Kada za Afya - 1,060 na Kada nyinginezo - 1,871)** walisimamishiwa mishahara na waajiri wao. Hata hivyo, idadi hii (7,382) ilichanganya Watumishi ambao hawakuwa na sifa, Watumishi waliokuwepo kabla ya

tarehe 20 Mei, 2004 pamoja na wale waliolegezewa masharti ya Muundo na Mkuu wa Utumishi wa Umma yaani Katibu Mkuu Kiongozi kupitia barua ya Katibu Mkuu Utumishi yenye Kumb. Na. CCB.271/431/01/P/13 ya tarehe 30 Juni, 2011.

**Mheshimiwa Spika;**

**5.** Pamoja na maelekezo hayo **sahihi ya Serikali** yaliyotolewa mara kwa mara, kumejitokeza malalamiko ya kutozingatiwa kwa maelekezo hayo wakati wa utekelezaji. Malalamiko hayo yamepokelewa na Ofisi yangu kutoka kwa **Watumishi walioathirika pamoja na Vyama vya Wafanyakazi.** Aidha, Serikali imepokea Ushauri na Maoni kutoka kwa **Waheshimiwa Wabunge katika Mkutano wa Bunge unaoendelea. Kutokana na hali hiyo, Serikali imeamua na inaagiza kama ifuatavyo:-**

**a)** Watumishi wote ambao walikuwa na **Ajira za Kudumu au Ajira za Mikataba (Kwa Watendaji wa Vijiji na Mitaa) au Ajira za Muda *(Employment on Temporary Terms)*** ambao walikuwa kazini kabla ya tarehe 20 Mei, 2004 ulipoanza kutumika Waraka wa Utumishi (Establishment Circular) Na. 1 wa Mwaka 2004, **Warejeshwe kazini mara moja, walipwe mishahara yao kwa kipindi chote ambacho walikuwa wameondolewa kazini na waendelee na ajira zao hadi watakapostaafu kwa mujibu wa Sheria**;

**b)** Watumishi wa Umma Elfu Moja Mia Tatu Sabini **(1,370)** waliolegezewa Masharti ya Sifa za Muundo kupitia Barua ya Katibu Mkuu Utumishi yenye Kumb. Na. CCB.271/431/01/P/13 ya tarehe 30 Juni, 2011, **Warejeshwe kazini mara moja, walipwe mishahara yao kwa kipindi chote ambacho walikuwa wameondolewa kazini na waendelee na ajira zao hadi watakapostaafu kwa mujibu wa Sheria**;

**Mheshimiwa Spika;**

**c)** **Uamuzi huu uliotajwa katika aya namba 5. (a) na (b) hapo juu hautawahusu Watumishi wa makundi yafuatayo;**

**i.** Watumishi waliowasilisha vyeti vya kughushi katika kumbukumbu za ajira yao;

**ii.** Watumishi waliokuwepo katika ajira kabla ya tarehe **20 Mei, 2004** ambao katika kumbukumbu zao rasmi kama vile taarifa binafsi

***(Personal Records),*** fomu za tathmini ya utendaji kazi ***(OPRAS)*** n.k walijaza taarifa za uwongo kwamba wanayo elimu ya kidato cha nne lakini wakashindwa kuthibitisha kwa kuwasilisha vielelezo vya sifa hizo kwa mujibu wa Miundo yao ya Utumishi;

**iii.** Watumishi wote waliioajiriwa baada ya tarehe 20 Mei, 2004 wakiwa hawana sifa ya kufaulu mtihani wa kidato cha nne kwa kuwa walijipatia ajira kinyume cha maelekezo ya Serikali;

**d)** Watendaji Wakuu na Wakuu wa Idara za Utawala na Utumishi wote walioshiriki kuwaajiri Watumishi wasiokuwa na sifa ya kufaulu mtihani wa kidato cha nne katika Utumishi wa Umma **baada ya tarehe 20 Mei, 2004** watachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu; na

**e)** Watendaji Wakuu na Maafisa wote wanaosimamia zoezi hili ambao kwa namna yoyote ile watashiriki kuhujumu zoezi hili kwa kuondoa au kuharibu kumbukumbu za Watumishi ili haki isitendeke,watachukuliwa hatua za kinidhamu na za Kijinai ikibidi.

**Mheshimiwa Spika naomba kuwasilisha.**

*Kapt (Mst*) George H. Mkuchika (Mb.)
WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS
(MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA)

***09 Aprili, 2018***